RICHLAND ONE
DEPARTMENT OF WORLD LANGUAGES AND ESOL PROGRAMS

2612 Covenant Road • Columbia, South Carolina 29204
Office: (803) 212-1475 .Fax: (803) 252-2951

Ernesto Bernal
Coordinator

Mei 10, 2019

Kwa Mzazi au Mlezi wa _____

KUH: Upanuzi wa Shule za Vituo vya ESOL 2019-2020

Ndugu Bwana au Bibi:

Wilaya ya Shule ya Richland One inajitolea kutoa ubora wa elimu wa kiwango cha juu kabisa kwa kila mwanafunzi kwenye wilaya yetu na kwa wakati huo huo, kukidhi miongozo yote ya jimbo na shirikisho ya kuhudumia familia zenye watoto ambao wameteuliwa kuwa ni wanafunzi wa Kiingereza. Idadi ya wanafunzi wa ESOL inaongezeka kwenye jimbo letu na wilaya yetu.

Kama sehemu ya ukaguzi upya wa makini wa shule zilizoteuliwa kama vituo vya ESOL, Richland One inapanua idadi ya vituo ili kukidhi vizuri zaidi mahitaji ya wanafunzi wetu. Sasa tutakuwa tunatoa huduma za ESOL kwenye shule zaidi ambayo itahakikisha kuwa watoto wanatumia muda kidogo kusafirishwa kutoka kwenye shule iliyowekewa sehemu hadi kwenye kituo cha ESOL na itawarudisha watoto kwenye jamii zao wawe karibu na nyumbani.

Unapokea barua hii kwa sababu upanuzi wa idadi ya vituo vya ESOL unamuathiri mtoto wako. Chati iliyoambatishwa inaonyesha vituo vya ESOL vya wilaya na shule ibukizi za kila kituo. Wanafunzi ambao kwa sasa wanahudhuria A.C. Flora ili kupata ufuatilizi na huduma za ESOL hawatolazimika kuhudhuria mojawapo kati ya vituo vipya vya shule za upili vya ESOL na wataruhusiwa wahitimu kwenye A.C. Flora isipokuwa ikiwa wazazi wanataka mtoto wao ahudhurie kituo cha ESOL kilichoko karibu na nyumbani kwao.

Rasilimali ambazo Richland One zinatoa kwa wanafunzi wa Kiingereza hazitobadilika wakati upanuzi huu unatekelezwa. Tutaendelea kuhakikisha kuwa walimu kwenye wilaya wanafunzwa, wanatayarishwa na wanajitolea kumhudumia mtoto wako na kutoa ufikiaji sawia wa fursa zinazopatikana kwenye wilaya yetu.

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu upanuzi wa shule za vituo vya ESOL, tafadhali zuru tovuti ya Richland One chini ya Idara ya Miradi ya ESOL. Hapo utapata hati yenye mada *Maswali Yanayoulizwa Sana ya Upanuzi wa Shule za Vituo vya ESOL*. Pia unaweza kupokea maelezo ya ziada kwa kupigia simu Kituo cha Kimataifa cha Kukaribisha (803) 212-1475 baina ya 9:00 AM – 12:00 PM mchana, Jumatatu hadi Alhamisi.

Kama kawaida, Wilaya ya Shule ya Richland One inathamini athari ya mtoto wako na familia yako kwenye shule zetu na jamii yetu. Asante kwa makini yako na kwa kutuunga mkono kwenye jambo hili. Tunatarajia fursa mpya kwa wanafunzi wetu ambazo zitaletwa na mwaka wa shule wa 2019-2020.

Kwa dhati,

Ernesto Bernal
Mratibu wa Lugha za Ulimwengu na Miradi ya ESOL